# K.C.P.E EXCEL SERIES

## DARASA LA NANE MUHULA WA TATU - 2014

## KISWAHILI: LUGHA

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

I) JINA LAKO  II) JINA LA SHULE YAKO  III) NAMBARI YA MTIHANI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Kwa kila nafasi chagua jibu lifaalo zaidi.***

Tezi alijiona sasa ni __1__ aliyebaleghe. Akaona ni wakati wa __2__ mwenyewe __3__ mema na mawi. Jambo la kwanza lililonijia akilini __4__ kutafuta njia ya kujitenga na aila __5__. Sio kujitenga kiasi cha __6__ lakini alitaka akae peke yake ili aweze kujiamulia __7__ bila ya kubughudhiwa na mtu. Alichoshwa kabisa na kazi za nyumbani.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | kijana | ajuza | shaibu | mtoto |
| 2. | kuchagua | kujichagulia | kumchagulia | kujichagua |
| 3. | kutokana na | katikati ya | katika | kati ya |
| 4. | ilikuwa | kilikuwa | lilikuwa | alikuwa |
| 5. | wake | lake | chake | yake |
| 6. | jua na giza | ardhi na mbingu | juu na chini | sahani na kawa |
| 7. | atakalo | atakaye | atakayo | atakacho |

Mchezo wa __8__ kati ya wachuuzi na askari wa __9__ la Nairobi unaelekea kufika __10__ baada ya wachuuzi kupewa __11__ vya kuendesha biashara hizo mbali na kutengewa sehemu maalum za shughuli zao. Kwa sasa hali ya utulivu katikati mwa jiji __12__. Lakini sio kwa muda mrefu, hali ya vurugu __13__ jiji. Wachuuzi walemavu __14__ dhulma dhidi yao waliandamana hadi ikulu ya Nairobi wakitaka __15__ awatetee.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 8. | watoto | paka na panya | sungura na mbwa | siafu na mende |
| 9. | kikosi cha jiji | baraza la wazee | baraza la jiji | kikosi cha askari |
| 10. | kikomo | mwanzo | kilele | mbali |
| 11. | mbali | vibali | ruhusa | idhini |
| 12. | wanarejea | limerejea | umerejea | imerejea |
| 13. | iliondoka | ulitanda | ilitanda | ilitulia |
| 14. | waliopiga | waliopinga | wanaohoji | wanaotaka |
| 15. | mbunge | seneta | gavana | rais |

***Kutoka swali 16 - 30, chagua jibu sahihi kulingana na maelezo.***

16. Ki imetumikaje katika sentensi hii.
Ukiuliza swali nitakujibu.
A. Kuonyesha hali ya masharti
B. Kuonyesha hali ya kukanusha
C. Kuonyesha hali ya kuendelea
D. Kuonyesha hali ya udogo

17. Chagua kikundi cha madini pekee.
A. Yakuti, zumaridi, lulu, titani
B. Afu, kilua, mkandi, wandari
C. Zabaki, mshtarii, zuhura, kausi
D. Ghuba, rais, gema, kisiwa

18. Chagua maelezo yasiyotoa maana ya neno kiboko.
A. Mjeledi uliotengenezwa kwa ngozi
B. Kitu kizuri cha kuvutia sana
C. Aina ya kipimo cha kitambaa
D. Nakshi ya shingoni mwa kanzu

19. Geuza kwa usemi halisi.
Kaka alikataa kunywa chai nyingine siku hiyo.
A. "Sitakunywa chai nyingine siku hiyo," kaka alikataa.
B. "Sitakunywa chai nyingine leo!" kaka alisema.
C. "Sitaki chai nyingine leo," kaka alikataa.
D. "Sitaki chai nyingine siku hii," kaka alisema.

20. Ni msemo upi unaotoa maana ya, kumsababishia mtu fujo?
A. Kumwonea kijicho
B. Kumlilia ngoa
C. Kumbwagia zani
D. Kumvika kilemba cha ukoka

21. Chagua sentensi iliyotumia kivumishi cha idadi.
A. Wanafunzi wengi watafanya mtihani.
B. Kiranja mwingine atachaguliwa
C. Chepeo chake kimeraruka
D. Mzigo huu ni wa nani?

22. Tambua sentensi sahihi.
A. Ebo! Hilo ndilo suluhisho pekee.
B. Mtume! Tumeshinda mechi hiyo.
C. Hamedi! Utagongwa na baiskeli.
D. Hario! Amenyang'anywa kibeti.

23. Mchezo wa watoto wa kurusha vijiwe na kuvitoa mashimoni huitwaje?
A. Kodwa B. Kibemasa
C. Foliti D. Gungwi

24. Maana ya methali Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi ni ________
A. jambo ambalo unaliona rahisi kwako kwa mwenzako huenda likawa gumu
B. haifai kudharau kitu chako duni kwa kutamani cha mwenzako
C. haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali huenda ukawahitaji baadaye
D. kiti unachokiona duni kwako huenda kikawa na manufaa kwa mtu mwingine

25. Khadija ni mkewe Ali. Juma ni kaka yake Khadija. Je, Ali atamwitaje Juma?
A. Mwanyumba B. Wifi
C. Mwamu D. Mjomba

26. Kifaa cha kielekroniki ambacho huongoza mitambo kutoka mbali huitwa ________
A. faksi
B. runinga
C. kisengeretua
D. nukulishi

27. Chagua orodha ya viunganishi vya kuongeza.
A. Isitoshe, licha ya, pia
B. Kama, ikiwa, lai
C. Lakini, isipokuwa, ingawa
D. madhali, maadamu, kwa sababu

28. Aina ya shairi lisilokuwa na vina vya ndani ambalo aghalabu huelezea wasifu huitwa ____
A. utenzi B. tathmina
C. tathmina D. mloto

29. Chagua sentensi inayoonyesha hali isiyodhihirika.
A. Naja
B. Tutaenda
C. Ametoka
D. Tunaondoka

30. Tetemeko la ardhi huitwa ________
A. kabobo
B. zilizala
C. kimbunga
D. tsunami

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswaii 31 - 40.</u>***

Baba alishakufa na kuzikwa katika makaburi ya Lang'ata. Alipolazwa katika hospitali ya Kenyatta, hakutoka akiwa hai. Lile gonjwa lilimtafuna mpaka likammaliza kabisa.

Hakuna aliyeshangazwa na kifo chake kwa sababu kilitarajiwa. Tuliishi katika enzi ya UKIMWI ambapo kifo hakikuwa mbali na uhai tena. Daima kilielea angani. Mara kwa mara kilichupa ardhini na kutwao mgonjwa wa Ukimwi. Ni kama vile tai anavyochupa kutwaa vifaranga. Jiji la Nairobi lililoa kifo, nchi nzima ilitikiswa na vifo vya Ukimwi. Hakuna hotuba ya kisiasa iliyokosa kuzungumzia tanzia hii. Viongozi wote kutoka rais, mawaziri, wabunge, wakuu wa makanisa na wataalamu mbalimbali. Waliungana na wananchi katika kilio cha kitaifa. Kifo cha babangu kilikuwa pigo kubwa sana kwetu. Kifo kilipomchukua ndipo tulipofungua alivyokuwa nguzo yetu pamoja na udhaifu wake wote. Sasa tulijikuta ka vifaranga ambao mama yao alishatwaliwa na nguchiro. Hata mahali pa kujikinga jua na mvua hatukuwa napo tena. Tulitakiwa kuihama ile nyumba tuliyoishi katika kituo cha polisi cha Bondeni. Tulipewa mwezi mmoja kutafuta mahali pengine pa kuishi. Hatukujua twende wapi.

Kilicholeta nuru hafifu ya matumaini katika mashaka yote hayo ni uchunguzi wa kimatibabu uliofanyiwa mama. Damu yake ilipimwa mara mbili, ikathibitishwa kwamba hakuwa ameambukizwa viini vilivyohusishwa na ugonjwa wa Ukimwi. Tulishukuru kwamba hata kama tulimpoteza baba, ugonjwa wake haukumvuta mama kaburini. Umaskini uliotusakama na msiba uliotulemea haukuvunja tamaa yetu ya kuendelea kuishi.

Kwa nyingine Padre Giovanni alitutendea fadhila kubwa. Alikuwa akifuatilia dhiki zetu tangu dadangu Freda alipojiunga na Misheni. Baba alipolazwa hospitalini alikuwa akienda kumwuguza na kumwombea mara

kwa mara, na ndiye aliyemshawishi mama kwenda kupimwa. Hata mazishi ya baba, ndiye aliyeyafanyia ibada ya kikatoliki. Alipofahamu jinsi tulivyokabiliwa na shida ya kupata mahali pa kuishi, alimtafutia mama kazi katika Misheni. Kazi ndogo tu ya kupalilia maua na kukata nyasi. Mama alipoanza kuifanya kazi hiyo alipewa chumba cha kuishi akahamia humo. Tatizo likabaki upande wangu. Nisingeweza kumfuata mama. Tusingeweza kuishi pamoja katika chumba kimoja tu alichopewa. Swaleh ndiye aliyeniokoa. Alinikaribisha kuishi pamoja naye katika chumba chake cha pale kituoni. Nyumba yao ilikuwa kubwa na kila mmoja alikuwa na chumba chake. Basi nikahamia huko, kujipa muda wa kufikiria la kufanya.

31. Kwa nini kifo cha babake msimulizi hakikuwa cha kushangaza?
    A. Babake alikuwa mtu mwovu aliyefaa kufa
    B. Alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu kabla ya kifo chake
    C. Alikuwa amelazwa hospitalini
    D. Alikuwa amemtaliki mamake mwandishi
32. Katika taarifa ulioisoma ni nini kinachofananishwa na tai?
    A. Nguchiro
    B. Mauti
    C. Ukimwi
    D. Dhiki
33. Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa jiji la Nairobi lililoa kifo?
    A. Kifo kilikuwa kwa wingi kama maji
    B. Kifo kiliwatosa wengi katika Ukimwi
    C. Ukimwi ulikuwa umesababisha vifo vingi
    D. Watu wengi wa jijini walikufa maji
34. Chagua sentensi inayoonyesha kuwa Ukimwi lilikuwa janga la kitaifa?
    A. Wataalamu mbalimbali waliungana katika kilio hicho cha kitaifa
    B. Nchi nzima ilitikiswa na vifo vya Ukimwi
    C. Kama vile tai alivyochupa kutwaa vifaranga
    D. Daima kilielea angani
35. Kwa nini msimulizi alikosa mahali pa kujikinga jua na mvua?
    A. Chumba chao kilikuwa kidogo sana
    B. Frida alikuwa katika Misheni
    C. Baba yake alikuwa amekufa
    D. Chumba chao kilitwaliwa na serikali
36. Chagua kauli sahihi.
    A. Mama yake msimulizi alikuwa na virusi vya Ukimwi
    B. Msimulizi aliishi Lang'ata
    C. Babake msimulizi aliifaa familia yake licha ya udhaifu
    D. Swaleh alikuwa na nyumba kubwa aliyoimiliki mwenyewe
37. Mama yake msimulizi alipewa kazi zifuatazo ila
    A. kutunza bustani
    B. kung'oa magugu na makwekwe baina ya maua
    C. kuongoza misa za kikatoliki
    D. kunadhifisha kiunga
38. Msimulizi anatoa sababu gani za kutomfuata mamaye.
    A. Mama yake alikabiliwa na dhiki nyingi
    B. Chumba alichopewa mamaye kisingewatosheleza wote wawili
    C. Swaleh alikuwa radhi kumsaidia
    D. Alikuwa na familia kubwa
39. Kwa nini mama alifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu mara mbili?
    A. Padre alimshawishi
    B. Kuthibitisha kuwa hakuwa na viini vya Ukimwi
    C. Kumtibu dhidi ya makali ya Ukimwi
    D. Kumkinga dhidi ya Ukimwi
40. Kitendo cha Swaleh kwa msimulizi kinaweza kuelezewa kwa methali kuwa ______
    A. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
    B. Kikulacho ki nguoni mwako
    C. Mwenzako akinyolewa tia chako maji
    D. Mvumilivu hula mbivu

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.</u>***

Tayari zaidi ya miongo mitano imepita tangu tujinyakulie uhuru kutoka kwa mabeberu. Wakoloni walipofunganya virago na kujiendea zao, sisi Waafrika tulichukua usukani. Malengo yaliwekwa na mikakati ya kufuatwa ikatayarishwa.

Malengo yaliyopewa kipaumbele ni kuondolea mbali ujinga na upuuzaji, kuangamiza ukali na maradhi kwa kuwapa raia wetu mahitaji ya kimsingi. Maneno kama vile "Maji kwa wote kufikia ......" yalisikika kila kukicha. Watawala kwa watawaliwa wakawa na matumaini makuu. Lakini leo hii mambo ni tofauti. Ingawa

kama taifa tumepiga hatua kadhaa katika nyanja mbalimbali bado malengo yetu ya wakati wa uhuru hayajatimia.

Polepole mambo yalianza kwenda upogo. Meli yetu ikaanza kuyumbayumba. Matumaini ya wazalendo ya kufika ng'ambo ya pili na ng'ambo ya ustawi na ustaarabu yakaanza kudidimia. Nafasi ya uzalendo ilichukuliwa na ubinafsi. Abiria wa meli wakaanza kuzozana. Wengi wakaugua saratani ya ukabila. Ni bayana utengamano uondokapo hupisha udororaji na masaibu tele.

Hatima ya yote hayo, mambo yamezidi kutokota. Umaskini umekita mizizi. Zaidi ya asilimia sitini ya wananchi wanaishi katika kitovu cha umaskini, umaskini wa kupindukia. Maji safi na salama ni neno geni kwa wengi nchini. Wengi wanazidi kusumbuliwa na maradhi kama vile homa ya matumbo na kipindupindu. Utapia mlo umewaathiri wengi. Miundo msingi inazidi kusambaratika. Ajira nayo inazidi kuadimika. Vijana wengi wanazidi kukanyanga lami licha ya kuwa na vyeti vya elimu na hata taaluma mbalimbali. Ni sharti tupige darubini kama taifa tuone ni wapi tulipotezea shabaha. Kisha tupige msasa. Ukweli ni kuwa tunao uwezo wa kupiga hatua mbele. Mradi tu tushirikiane. Tuelewe kuwa nia zikiwa pamoja, kilicho mbali huja karibu.

41. Chagua orodha ionyeshayo mahitaji ya kimsingi pekee.
   A. Lishe bora, usalama, madaraka
   B. Usalama, chakula, makao
   C. Makao, elimu, starehe
   D. Mavazi, chakula, ushirikiano

42. Pindi tu wakoloni walipoondoka humu nchini
   A. wananchi walipewa mahitaji ya kimsingi
   B. mikakati ya kufikia ufanisi zaidi iliwekwa
   C. malengo yalishughulikiwa kwanza
   D. uhuru ulipatikana

43. Kwa mujibu wa taarifa uliyoisoma ________
   A. nchi yetu haijapata maendeleo yoyote
   B. nchi yetu haijaafikia malengo mengi ya hapo awali
   C. Nchi yetu haina maji safi na salama
   D. Kwa kiasi fulani nchi imejikwamua kutokea kwa umaskini

44. Mambo nchini yalianza kuharibika lini?
   A. Pindi tu mabeberu walipoondoka nchini
   B. Meli ilipoanza kuyumbayumba
   C. Pindi Wafrika walipoanza kujitawala
   D. Ubinafsi na maovu mengine yalipowakumba wananchi

45. Nafasi ya uzalendo ilichukuliwa na ubinafsi. Nini maana ya kifungu hiki?
   A. Watu waliacha kufikiria matakwa ya nchi badala yake wakajifikiria wenyewe zaidi
   B. Watu walianza kusaidiana wao kwa wao
   C. Watu walishirikiana katika ujenzi wa nchi
   D. Wazalendo walikuwa watu binafsi

46. Kutokana na kifungu abiria wa meli inayozungumziwa ni kina nani?
   A. Raia
   B. Viongozi
   C. Mabeberu
   D. Maskini

47. Ugonjwa wa homa ya matumbo husababishwa na ________
   A. ukosefu wa lishe bora
   B. utumiaji wa maji na chakula kichafu
   C. vidudu viishivyo katika maji ya vidimbwi
   D. kupumua hewa yenye uchafu

48. Mwandishi anapendekeza tufanye nini ili kuzikabili dhiki zetu?
   A. Tuwe na nia moja tu
   B. Tuondolee mbali ubinafsi
   C. Tujikinge kutokana na maradhi
   D. Tuishi kwa imani

49. Ukosefu wa utengamano husababisha ________
   A. uchochole
   B. ukoloni
   C. saratani
   D. ufanisi

50. Chagua kauli sahihi kwa mujibu wa taarifa.
   A. Hakuna matumaini yoyote ya kuyafikia malengo yetu
   B. Msimulizi ni mzalendo kamili
   C. Wakoloni wanafaa kulaumiwa kwa masaibu yetu
   D. Wananchi wengi wanaugua saratani